Muungano wa Kimataifa wa Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu (IFRC).

Mwongozo wa kuendesha mazungumzo ya kikundi cha wanajamii wanoajitolea

Mawasiliano juu ya hatari na ushirikishwaji wa jamii kwa virusi mpya ya corona

Nakala: 05/03/2020

Sababu

Nia ya mwongozo huu wa mawasiliano ya hatari na mwongozo wa ushiriki wa jamii ni kukusaidia kuendesha maongezi ya kikundi na watu wanaojitolea kwa jamii kuelewa maulizo, bongo, maoni na wasiwasi wanaosikia juu ya virusi mpya ya corona kutoka kwa batu wakati wa kazi zao katika jamii. Wanaojitolea wanaishi na kufanya kazi katika jamii na kwa hivyo ni batu ya muhimu bakutosha ako habari za mupya na mawazo yenyi inatembea juu ya virusi mpya ya corona (pia inaitwa COVID-19) katika jamii. FGD hii pia ni wakati ya kuambia kwa wafanyakazi wakujitolea wa kijamii kuhusu habari muhimu ya kiafya kuhusiana na ugonjwa ya virusi mpya ya corona na kusisitiza kazi muhimu wanaofanya kukusanya maoni kutoka kwa jamii, ambayo inaweza kutumika kufanya majibu zikuwe muzuri zaidi. Maulizo zimoya ni za nguvu sana na kwa hivyo inapashwa kuulizwa kwa uangalifu na kulingana na asili ya nyumbani.

Mazungumzo ya kikundi ni nini?

Mazungumzo ya kundi (FGD) ni njia ya kukusanya habari ya ukweli inayowaleta batu kutoka kwa jamii kuzungumzia maongezi fulani. Maulizo ziko wazi, kwa nia ya kufanya mazumgumzo ya kawaida na washiriki ju baelewa maoni yao, imani, wasiwasi, maulizo na mahitaji ya habari yenyi inaangaliana na muripuko wa corona. FGD inachukuwaka karibu saa moja na inafaa kukuwe yulu ya batu 8 na bila kuzidi batu 12. Ni ya muzuri kuwa na FDG tafauti ya wanaume na wanamuke. Hii itawasaidia kutoa maoni yao waziwazi. Kama wakati hairuhusu, unaweza kuwa na ya kuchangana (nusu ya wanaume na nusu ya wanamuke).

Nani anaweza kuongoza mazungumzo ya kundi?

Kuko kazi mbili yanayotakiwa kufanya mazungumzo ya muzuri ya kundi: muongozi na mwandikaji. Ikiwezekana, muongozi na mwandikaji banapashwa kuwa bote ba kiume wala kianamuke kufuatana na washiriki.

Muongozi – lazima awe mtu anayezungumza lugha ya wenyeji mwenye anaongea muzuri na kuweza kufanya watu wajisikie kufurahia. Katika hali zingine ikiwa muongozi hazungumzi lugha ya wenyeji, wanaweza kufanya kazi na mtafsiri (interprete). Muongozi anahitaji kuweza kuchunguza zaidi kufuatana na majibu yaliyopokelewa ao kuuliza tena maulizo kama batu habakuelewa.
Lazima pia waweze kuweka washiriki mu ile maongezi na kuhakikisha kwamba kila mtu anaweza jisemeya.

Muongozi mzuri anapashwa:

- ✔ Kuelewa mzuri maulizo ya FGD na ujumbe za muhimu za COVID-19
- ✔ Akuwe msikilizaji mzuri na kuoneshe huruma kwa washiriki
- ✔ Epuka maulizo za kuongoza, usikuwe wa ngambo ya mtu na usiseme kitu ku majibu ya washiriki ju usipate habari za bongo mu maongezi
- ✔ Maulizo zimoya ni za makali sana, waulize kwa heshima na kulingana na asili

Mwandikaji – lazima aweze kuzungumza na kuandika kwa lugha ya kienyeji ju aandike mazungumzo ya kundi vema. Pamoja na kuandika kile kinachosemwa wakati wa mazungumzo ya kikundi, mwandikaji pia anapashwa andika tabia ya washiriki (mita zamo ya kushangaza, majibu ya haraka, maingiliano kati ya washiriki, na bingine). Mwandikaji anapashwa kudumisha siri wakati wa kuandika maongezi mu kutumikisha herufi ao nombre kutambua washiriki pahali ya majina. Mwandikaji anaweza kuamua kuandika maneno za kidogo tu wakati wa maongezi lakini nyuma tu ya maongezi, anapashwa kuandika maelezo kwa undani ju habari zote za lazima ziandikiwe.

Mwandikaji mzuri anapashwa:

- ✔ Kujuwa sana gisi ya kusikiliza na kuandika
- ✔ Kukuwa na ufahamu ya maulizo na maongezi ya kuchunguza
- ✔ Andika bienye batu baneza sikia muzuri lakini apana kila kitu
- ✔ Asikuwe na ubaguzi
- ✔ Uliza, kwa makubaliano ya muongozi, mshiriki kurudilia jibu yake kama hakusikia mara ya kwanza.



Mapendekezo ya namna ya kuikala wakati wa mazungumzo ya kikundi

Mbele	Wakati	Kisha
✔ Panga ju ya nia, mwongozo wa maongezi, gisi ya kuchagula washiriki, wakati na fasi ✔ Fahamisha viongozi wanaofaa na viongozi wanaojitolea kama munaendesha FGD ✔ Hakikisha ile fasi ni rahisi kuifika ako na wanaojitolea wanajisikia vizuri.	✔ Muambiyane majina ✔ Fasiria uko nani na nia na muda wa FGD ✔ Omba ruhusa ya kuandika na ueleze kama siri itakuwa kwa muda wote ✔ Shukuru kila mtu kwa ushiriki wake.	✔ Ku mwisho, wape wakati wale wakujitolea kuuliza maulizo yao wenyewe na kufasiria washiriki bienye utafanya na maandiko ile ✔ Muongeye pamoja na andika habari yoyote ya zaidi haraka iwezekanavyo ili usisahau.

Mwongozo wa maulizo wa FGD na batu wanaojitolea kwenye jamii juu ya virusi mpya ya corona

JINA LA TAWI: _____

Municipalité/District//commune: _____

Tarehe: (DD/MM/YYYY) ____ / ____ / _____

Waongozaji wa Msalaba Mwekundu/Hilali Nyekundu: _____

Jina la kikundi/maelezo: _____

 # ya washiriki wanaume: _____ **# ya washiriki wanamuke:** _____

Je, vikundi vilivyo hatarini vilikuwa (wazee, walemavu nk)? _____

Utambulishaji na makubaliano

Utambulishaji wa jumla:
Habari ya asubuhi/mchana, jina yangu/yetu ni _____. Tunafanya kazi na [Shirika la Kitaifa] Msalaba Mwekundu/Hilali. Tuko hapa na Kitengo yako ya nyumbani kusikia byenye batu katika jamii yako banasema juu ya ugonjwa ya virusi mpya ya corona, ambayo pia inaitwa COVID-19. Tunaweza kutumikisha habari hii kupanga majibu ya société Nationale kwa virusi mpya ya corona na kuhakikisha kuwa jamii zinapata habari za ukweli zinazo shughulikia wasiwasi yabo, hofu na habari za bongo. Sawa gisi mtu wa kujitolea kwa jamii, uko mutu mwenye anaweza pana habari juu ya bienye biko napitikana ndani ya jamii yako. Ku mwisho tutashiriki habari ya ukweli juu ya ugonjwa wa virusi ya corona na alama zake.

Uko _____na dakika za kujibu batu katika iyi mazungumzo?

Uko na maulizo yoyote?

MAKUBALIANO:

Unapana makubaliano ya kuandikisha, kutumikisha, kuweka na kugabula habari iliyotolewa kwa kuripoti na mawasiliano?

☐ NDIO ☐ APANA (ikiwa APANA, sema asante na umalize maongezi)

Unapana makubaliano ya kukamata, kutumikisha, kuweka na kugabula picha yako kwa ripoti na mawasiliano?

☐ NDIO ☐ APANA (Ikiwa APANA, usipige picha ya mtu huyo na umuombe kama unaweza kuendelea na maongezi)

Naweza kuanza sasa?

ULIZO	JIBU
UFAHAMU	
Je, ni vitu vya aina gani watu wanasema katika jamii yako kuhusu ugonjwa mpya wa corona? Tafazali hesabu majibu - pamoja na ikiwa watu hawaya bisikia.	
Je, unaulizwa maulizo gani kuhusu ugonjwa mpya wa corona? Tafazali hesabu majibu.	
Je! Ni wapi na kutoka kwa nani jamii inapataka habari zao juu ya ugonjwa mpya wa corona? Tafazali hesabu majibu.	
Kufuatana na jamii, mtu anaweza kupata ugonjwa mpya wa corona aye? Chunguza imani: akili, kutonawa mikono, kula chakula zimoya, kutoka kwa kikundi fulani cha watu, ma nyama, kugusa wengine, kukohoa, kupiga chafya, na bingine.	

Je, batu banawazaka inaambukiaka/ kupita kutoka kwa mtu moja kwenda kwa mwengine?	
Kwa maoni yako, kuna vikundi vya watu ambao wako katika hatari zaidi kuliko wengine kwenye jamii yako? Kwa mfano, watoto, wazee, watu ambao tayari ni wagonjwa, wahamaji na wakimbizi, wanaume, wanamuke na bengine.	
Kufuatana na bye umeona na kusikia katika jamii yako, batu banajua alama za ugonjwa mpya wa corona? Tafazali hesabu majibu	
Batu banajua kipindi ya incubation ya corona ni nini? Hii inamaanisha urefu wa muda inachukua kwa mtu kuonyesha alama za ugonjwa mara tu wanapoambukizwa na virusi.	

Batu banasemaka nini itafikia mtu ambaye amepata corona? Hii ni kuelewa gisi batu banawaza ju ya iyi virusi	
Ulishaka sikia ju ya kutenga mtu mwenye banashakia kukuwa na ugonjwa? Unajua hii inamaanisha nini?	
Watu katika jamii yako wanaweza sikia aye ju ya kutenga watu ambao ni wagonjwa?	
Batu katika jamii yako wanalaumu kikundi fulani cha watu kwa kusambariza virusi? Ikiwa, ndio kwa nini wanafikiria hivyo? Hii ni juu ya kuelewa uwingi wa ubaguzi katika jamii	

TABIA ZA KUTAFUTA AFYA	
Ni njia gani njo batu banawaza banaweza kujilinda amo boye na ma familia zabo ku ugonjwa ya virusi ya mupia ya corona? Chunguza: matumizi ya waganga wa asili na dawa, kunawa mikono, kupiga chakula vizuri, kukaa mbali na batu, kufunika mdomo na kitambala ao ndani ya mukunjo ya kononngo wakati unapiga chafya ao kugohola, kusafisha vitu mara kwa mara kuuwa vidudu na bingine.	
Batu katika jamii yako bananawaka mikono yabo mara kwa mara? Ikiwa ndio, uliza kwa nini? Ikiwa apana, kwa nini?	
Je, watu wanaenda wapi wakiwa wagonjwa? Chunguza: banganga ba asili na ma dawa, maduka ya dawa/vituo vya matunzo, mashauri kutoka kwa viongozi wa dini na biongozi ya jamii, mashauri kutoka kwa serikali/UN/NGOs na bingine.	

Je, watu wangejua nini cha kufanya wakipata alama za ugonjwa sawa gisi homa/mafua yenye inaweza kuwa corona?	
MAWASILIANO	
Wapi njo fasi ya kwanza kwenye unatoshaka ma habari juu ya kujikinga na kutunza virusi ya mupya ya corona? Tafazali hesabu majibu.	
Je, gabulaka habari na jamii namna gani? Izi ma siku umetembelea nyumba ya mtu ao kufanya mikutano ya jamii? Kupitia njia ngani na ni nani anayeamua ni saa gani habari inapashwa kusambazwa kwa jamii	
Je, kila mtu katika jamii anapataka habari kuhusu ugonjwa ya virusi mpya ya corona? Chunguza: ni nani anashida ya kupata habari-wanamuke, watu wenye ulemavu (bilema), walio wachache na bengine.	

Je, unafikiriaje, kama sawa vile Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu, tunaweza kujibu ku corona?	
MAONI	
Je, ni nini njo habari za bongo zenyi zinavuma sana, maulizo, mashaka na boga juu ya virusi mpya ya corona yenyi inatembea katika jamii?	
Je, habari hii unapataje kutoka kwa jamii? Chunguza njia tafauti zinazotumikishiwa na batu banaojitolea kukusanya habari kutoka kwa jamii	
Kama wafanyakazi wa kujitolea, munafanya nini na habari munayosikia kutoka kwa jamii? Chunguza: gisi wanaojitolea wanashiriki habari kati abo benyewe, gisi wanajibu maulizo, kushughulikia habari za bongo, kushiriki na wafanyakazi	
Ikiwa jamii ina maulizo ao maoni kwa Société Nationale kuhusu corona, nini njo njia ya muzuri ya kufanya hivi? Uso kwa uso, kupitia kiongozi wa jamii, simu ya bila malipo, jumbe,	

mkutano wa jamii, kikundi ya jamii inayosimamia maoni, na bingine	
Je! Unafikiri wanajamii wanajua wana haki ya kutoa maoni, wapi na jinsi ya kufanya?	
KUSHIRIKI	
Je, Jamii yako inafanya kazi zozote kujiandaa na kuzuia virusi mpya ya corona? Tafazali eleza	
Kwa maoni yako, ni mipango gani za jamii ambazo unazani zinafaa zaidi kwa kuzuia corona? Chunguza: nguvu na uwezo ya wafanyakazi tafauti wa kujitolea, ni nini ilitumika mu siku za kupita kwa miripuko zingine za ugonjwa? Gisi wametumika na vikundi tafauti, gisi wanavyopanga mikutano yao ya jamii, kazi zao katika jamii? FGD kama iyi?	
Unaweza kutia aye jamii katika kupanga na kuendesha izi mipango?	
Unafikiria tunaweza kushirikiana na viongozi wa jamii na batu benye bana julikana sana kuzuia	

virusi mpya ya corona? Viongozi wa mitaa, viongozi wa vikundi, viongozi wa dini. Chunguza kile ambacho kimefanya kazi ao haikufanya kazi hapo mu wakati ya zamani	
UBAGUZI	
Je, umeona katika jamii yako ubaguzi wowote ya vikundi vimoya kutokana na corona?	
Uko na maulizo yoyote kwetu?	

Maliza

Kufuatana na ile maongezi, chukua wakati wa kuwapa watu wanaojitolea habari za mupia za afya kuhusu corona ukitumia mwongozo kutoka IFRC, OMS na UNICEF, ambayo inaweza kupatikana kwenye kitovu cha ushiriki wa jami (hapa). Wape washiriki vifaa vya IEC yoyote uliyonayo ikiwa ni pamoja na bitu bya muhimu na maongezi kwa wafanyakazi wa jamii, wanaojitolea na miungano. Unapashwa kufasiria:

- Virusi mpya ya corona ni nini, pamoja na ukali wa maambukizi
- Alama za virusi mpya ya corona
- Gisi ya kuambukia ya virusi mpya ya corona
- Matendo ya afya ya kuzuia maambukizi
- Matunzo
- Sema maswala yoyote ya ubaguzi
- Biombo bienyi biko byenyi binatumikishiwa na NS kukusanya na kujibu maoni
- Kwa kifupi ku bienye NS ikonafanya kwa ujumla kuzuia virusi ya corona

Asante sana kwa muda na maoni yako!